**JINA……………………………………………. NAMBARI YA USAJILI ……...…**

**MKONDO……………JINA LA SHULE……………………………………SAHIHI………**

**KISWAHILI**

**102/2LUGHA**

**MUDA: SAA $2^{1}/_{2}$**

# MTIHANI WA PAMOJA WA NYAHOKAKIRA AWAMU YA TATU, 2022

**Maagizo:**

a) Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, jina la shule yako na utie sahihi katikanafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Jibu maswali yote.
c) Maswali yote yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
e) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.
f) Watahiniwa ni lazima wahahakishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapasawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| **1** | **15** | |
| **2** | **15** | |
| **3** | **40** | |
| **4** | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata**

Siku ya pili ya Muna alikwenda kwao kushinda yeye na mumewe, kama desturi yao kila siku. Siku hiyo ilikuwa ikimpa fursa Muna ya kujipumzisha na kazi za nyumbani,akiwa amehesabiwa kuwa mgeni, kwa kuwa mama yake ndiye aliyefanya kazi zote, pia ilimpa fursa nzuri ya kuzungumza na wazee wake. Na saa za jioni, ambapo Hasani, mumewe hutoka kwa kutembea, Muna alichukua fursa hiyo kuzungumza na baba yake. Kwa Muna, mazugumzo hayo yalikuwa kama dawa kwa mgonjwa; humpa nafuu katika moyo wake na kumpa nafuu ya pumzi. Baba yake alimwuliza, ‘‘Je, vipi maisha yanaedelea?’’

Muna alijibu, ‘‘Yanaendelea vizuri. Ah, hivyo hivyo.’’ ‘‘Vipi?’’ Aliuliza baba yake, aliposikia sauti ya shaka katika maneno hayo.

‘‘Kwa kweli, wakati mwigine hujihisi kama niko peke yangu au kama mtu aliyepotea njia,’’

‘‘Namna gani?’’ aliuliza Saidi,

‘’Unasadiki, baba, tokea siku aliyonioa, sijapata hata siku moja kumwona Hasani akisoma gazeti au kukamata kitabu.’’

Baba yake alitabasamu na kusema, ‘‘Ina maana kuwa …’’ ‘‘Kuwa hatuna la kuzungumza zaidi ya yale mambo ya nyumbani,’’ alisema Muna kwa ukali. ‘‘Lakini, alisema Saidi kwa hadhari. ‘‘Labda Hasani ni kati ya wale wanaopenda kupata habari kwa kusikiliza redio au kutazama televisheni.’’ ‘‘Muna alitikisa kichwa: ‘‘Hasikilizi habari. Akifungua redio huwa kwa kusikiliza muziki, tena ule wenye ghasia nyingi. Na televisheni anaweza kuikalia hata kutwa, lakini muhimu kwake ni zile filamu za kupigana, za kitoto. Hawezi kuchagua.’’

‘‘Sikiliza Muna,’’ alisema baba yake, ‘‘Kila jambo linataka mazoea. Na wewe unaweza kidogo kidogo, si kwa nguvu wala kwa kumshikilia, lakini kwa wewe tu kuyafanya, ukamzoesha hayo yote.’’

Muna alitikisa kichwa: ‘‘Nimejaribu. Nikifungua tu televisheni kusikiliza habari au jambo la faida, ama ataifunga au kuondoka. Akiniona nasoma kitabu hunung`unika kuwa ninapoteza wakati wangu wote katika vitabu, na kadhalika. Ama nikinunua magazeti, husema ninapoteza pesa zangu bure tu kila siku. Ahh!’’ Muna alishusha pumzi, ‘‘Kwa hakika sijui nifanye nini.’’

‘‘Mchukulie kwa tabia yake. Usimulazimishe, maana mtu lazima aweze kupumzika na kustarehe nyumbani kwake. Akiona unataka kumlazimisha, atakereka na kuhamaki na kuzidi kukupinga. Muna alishusha pumzi tena, kwani aliona kuna kasoro kubwa katika maisha yake. Alikwisha zoea na kuelewa starehe ya kupitisha wakati wake katika vitabu na kujua yanayopita ulimwenguni. Kabla ya hapo alikuwa akizungumza na babake kuhusu yale aliyosoma au

kujifunza na kwa njia hiyo alishajiika na kuendelea zaidi. Baada ya kuolewa, alitumani kuweza kuzungumza na mumewe na akilini mwake alikuwa na picha ya wao wawili wakikaa kuzungumza mengi kuhusu haya na yale ndani ya vitabu, magazeti na televisheni. Lakini hayo hayakuwa, na ukosefu huo ulimwachia kiu kikubwa. Kwa hivyo ile ziara yao ya kila mwezi kwa wazee wake Muna ilimpa furaha kubwa.

Baba yake alimwangalia usoni kama anayejaribu kusoma fikra zake na kusema, ‘‘Unajua Muna kuna watu wa aina nyingi duniani, wanaume kwa wanawake. Lakini katika wakati huu tulio nao, wanawake wana shida kubwa.’’

‘‘Ninaelewa,’’alisema Muna, ‘‘Wanaume wengi kati ya watu wetu wanafikiri hapana haja ya mwanamke kupata elimu. Mwanamke kazi yake kukaa nyumbani, kupika, kufua, kuzaa, na kulea. Ana haja gani tena ya masomo? Hasa akiwa amekwisha jifunza kusoma na kuandika? Hayo yamtosha.”

Baba yake aliitikia kwa kichwa: ‘‘Nasikitika kusema hayo ni ukweli…’’ ‘‘Na akiwa ana akili nzuri, anatarajiwa aifiche, kama kwamba ni jambo la aibu kwake. Niambie baba, watu kama hao wanamtarajia mwanamke mwenye akili nzuri afanye nini?’’

Mara hii baba ndiye aliyeshusha pumzi, akielewa hamaki na uchungu wa Muna. ‘‘Ama ninavyofikiria ni kuwa watu kama hao wangefurahi kama mwanamke huyo ataitumia akili yake kwa kumtumikia na kumsaidia mumewe ili aendelee mbele afuzu katika maisha yake.’’

‘‘Ehe! Na yeye mwenyewe ? Ajisahau kabisa. Aishi chini ya kivuli cha mumewe?’’ ‘‘Muna, usisahau,’’ alisema baba yake, ‘‘Kuwa tunatoka mbali, na hivi karibuni tu ndiyo mwanamke ameweza kupata elimu ya juu, sawasawa na mwanamume. Hiyo walibidi wapiganie.’’

**MASWALI**

a. Kwa nini Muna hapendezwi na uraibu wa Hasani (alama 3)
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

b. Hasani hafurahikii mienendo ya mkewe. Thibitisha kwa hoja tatu (alama 3)
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

c. Mwandishi amefaulu katika matumizi ya kinaya kufanikisha kazi yake. Toa ithibati. (al 2)
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

d. Kando na babake Muna kumshauri, Taja sifa zingine alizo nazo. (alama 2)
………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

e. Taja kisababishi kikuu cha kiu kikuu ya Muna (alama 1)
……………………………………………………………………………………………

f. Taja faida mbili anazopata Muna anapowatembelea wazazi wake (alama 2)
………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

g. Eleza maana ya msamiati ufuatao namna ulivyotumika katika kifungu (alama 2)

(i) Alishajiika
……………………………………………………………………………………

(ii) kuishi chini ya kivuli cha mumewe
……………………………………………………………………………………

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

**<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali</u>**:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji

wataalamu mahususi. Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya ananchi wasio na hatia.Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

(a) Kwa maneno yasiyozidi **themanini**, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa.(alama 7)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. (alama 6)

**Matayarisho**

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.........................................................

**Nakala safi**

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Taja mifano miwili ya **sauti mwambatano** (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

b) Andika neno la Kiswahili lenye muundo ufuatao (alama 1)

Kipasuo-kwamizo cha kaakaa gumu

Irabu ya chini kati

Irabu ya mbele juu

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

c) Andika neno lenye viambajengo vifuatavyo : (alama 2)

Nafsi ya pili wingi

Mzizi

Kauli ya kutendesha

Kauli ya kutenda

'O'rejeshi tamati

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

d) Onyesha mzizi katika neno **kulipokuchwa** (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………….

e) Ainisha **vihusishi** katika sentensi zifuatazo (alama 2)

Walipalilia mahindi yao kwa mgwamba

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

Tumealikwa harusini na kasisi

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

f) Tunga sentensi moja iliyo na **kivumishi cha idadi jumla na kivumishi cha pekee** kuonysha badala ya (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………

g) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania katika ngeli ya U-U kutokana na neno zusha (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………

h) Andika sentensi ifuatayo *katika* ***waka*****ti ujao hali isiyodhihirika** (alama 2)

Mwanariadha anakimbia uwanjani.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

i) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa (alama 2)

Nguo ambazo zinauzwa katika duka hilo zinavutia.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

j) Kanusha sentensi ifuatayo (alama 2)

Naja uko sasa hivi ningoje.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

k) Andika kwa **usemi halisi** (alama 2)

Omari alishangaa na kusema kuwa wazuri hawakuwa wamezaliwa wakati huo baada ya kumwona kisura huyo.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………

l) Onyesha **kiima, yambiwa na yambwa** katika sentensi hii (alama 3)

Mwanafunzi alimfutia mwalimu wake ubao.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………

m) Bainisha **aina za vishazi** katika sentensi ifuatayo : (alama 2)

Ikiwa umetibiwa mbona mgongo bado unakuuma?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………

n) Tungia kirai kihusishi kama kielezi katika sentensi (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………

o) Kwa kutolea mifano kwenye neno onyesha miundo miwili **ya silabi wazi** (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa **njia ya mistari** (alama 3)

Uamuzi ambao umeafikiwa utawaridhisha.

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………..

q) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Mtoto alitimua mbio kuona nyoka.

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………….

r) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia **kinyume** **(**alama 1)

Mwanafunzi mwema anapenda kutii maagizo.

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

s) Onyesha matumizi ya kiambishi **-KU-** katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Asna atakutengenezea mpini wa jembe kasha aelekee kule kwao

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

t) Tunga sentensi mbili kudhihirisha matumizi mawili tofauti ya vifungo (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………

u) Eleza maana ya sentensi ifuatayo ikirejelea maneno yaliyopigiwa mstari (alama 1)

Mwenyekiti **alikunja jamvi** la mkutano huo.

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

v) Kichala ni kwa matunda nacho kilinge ni cha____________na ____________wa ndizi (alama 1)

**ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

Umealikwa kwenye kikao cha kamati ya nidhamu shuleni kujibu madai ya kuchochea wanafunzi kugomea mitihani. Andika sifa tano za lugha utakayotumia kujitetea. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………….

Sara katika maongezi yake anapenda kutumia viziada-lugha,eleza sababu ambazo huenda zikamfanya kuwa na hali hii. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………